

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 2322761-5  
Fax No. +255 026 2324218  
E-mail: [info@bunge.go.tz](mailto:info@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

Katika kutekeleza Masharti ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kuhusiana na umuhimu wa maoni ya Wadau katika mchakato wa uchambuzi wa Miswada ya Sheria katika ngazi ya Kamati za Bunge, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Thomas D. Kashillilah anautangazia Umma kwamba siku ya **Jumamosi, tarehe 01 Julai, 2017 kuanzia saa 3.00 asubuhi katika Viwanja vya Bunge Mjini Dodoma**, Kamati za Bunge zitafanya zoezi la **kukusanya maoni ya Wadau** mbalimbali kuhusiana na Miswada ifuatayo ya Sheria:-

- a) Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re- Negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017*];
- b) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017 [*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*]; na
- c) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

Kwa Tangazo hili, Wadau mbalimbali mnakaribishwa kwa ajili ya kutoa maoni yenu kwa kufika moja kwa moja katika Kumbi zilizopo katika Viwanja vya Bunge Mjini Dodoma (Ukumbi wa Msekwa na Ukumbi wa Zahanati Mpya) au kwa kutuma maoni yenu kwa Katibu wa Bunge kwa njia ya Posta au barua Pepe kupitia anuani ifuatayo:

Katibu wa Bunge,  
Ofisi ya Bunge,  
S.L.P 941,  
**DODOMA**  
Barua pepe: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano.  
Ofisi ya Bunge,  
**Dodoma**

29 Juni, 2017